

Wapendwa Wanafamilia na Wafanyakazi wa Cajon,

Kama sehemu ya huduma yetu kwa jamii, muungano wa shule wilaya ya Cajon Valley utatoa huduma bure za dharura za utunzaji wa watoto kwa wazazi wa wanafunzi wetu ambao ni wafanyakazi muhimu wakati wa dharura. Orodha kamili ya wafanyakazi muhimu wakati wa dharura kwa mpangilio inapatikana [hapa](#). **Tutakuwa tukifuata agizo la kiutendaji la Gavana Newsom na tutawapa kipaumbele wafanyakazi muhimu wakati wa dharura, kulingana na mpangilio wa orodha ya wafanyakazi muhimu.**

Ikiwa utapendelea kutumia huduma hii tafadhali jaza fomu ya usajili mtandaoni www.ezchildtrack.com/cajon/parent. Hakikisha unatumia kompyuta ya mezani au kompyuta ndogo ili kukamilisha usajili mtandaoni. Uthibitishaji wa ajira utahitajika wakati wa mchakato wa kusajili. Usajili wako ukikubaliwa, utaarifiwa na tarehe ya kuanza. Kama una maswali juu ya mchakato wa usajili tafadhali tutumie barua pepe edpadmin@cajonvalley.net

Kwa kweli, usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wetu utakuwa ndio kipaumbele cha juu wakati tunaendelea kupata habari za ziada kutoka kwa viongozi wa afya ya umma.

Kwa niaba ya Bodi yetu ya Uongozi na Wafanyakazi, asanteni wafanyakazi wetu wa muhimu wakati wa dharura wanaotoa huduma za utunzaji wa afya, usalama, chakula, miundombinu, wanaojibu wakati wa Dharura, na kazi muhimu ambazo sisi sote tunazihitaji wakati huu mgumu. Tunawashukuru kwa huduma zenu.